TANGAZO LA SERIKALI NA. 30 la tarehe 17/02/2017

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA 287)

# HATI RASMI

*(Imetungwa chini ya kifungu Na. 88)*

HATI RASMI (UANZISHAJI WA BODI YA HUDUMA ZA AFYA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE, 2017

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Hati Rasmi hii itajulikana kama Hati Rasmi (Uanzishaji wa Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri) ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, 2017 na itaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Hati Rasmi hii itatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.

Tafsiri

3. Katika Hati hii isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo:-

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

‘’ Kamati ya maendeleo ya kata ‘’ maana yake ni kamati iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 31 cha sheria ya Serikali za Vijiji (Mamlaka za Wilaya) Sura 287

“Kamati ya Kituo cha Afya “maana yake ni kamati iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 28(1) cha Hati Rasmi hii;

“Kamati ya Usimamizi ya Hospitali” maana yake ni kamati ambayo imeanzishwa chini ya kifungu cha 17 cha Hati Rasmi hii.

‘’ Kituo cha Afya, maana yake ni kituo cha kutolea huduma ya afya amabcho kiko ndani ya trafa, kinatoa huduma za afya kwa wagonjwa wa nje na waliolazwa pamoja na waliopewa rufaa toka kwenye zahanati ikiwa ni pamoja ya Mama na mtoto na kina uwezo wa Vitanda kumi na tano na kuendelea.

‘’ Kituo cha Huduma ya Afya cha Umma ‘’ maana yake ni kituo cha kutolea huduma ya afya kinasimamiwa na serikali.

‘’ Kituo cha Huduma za Afya cha shirika lisilo la serikali ‘’ maana yake ni kituo cha huduma za afya kinachomilikiwa na shirika au chama kwa misingi ya kujitolea na kutoa huduma na malipo bila faida na kinaendesha shughuli zake kwa kufuatana na kanuni na taratibu zilizowekwa na serikali.

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

‘’ Kituo cha Huduma za afya cha binafsi ‘’ maana yake ni kituo cha Huduma nza Afya kinachomilikiwa na kuendeshwa katika utoaji wa Huduma zake lengo likiwa ni pamoja na kupata faida.

‘’ Mkurugenzi ‘’ maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya au ofisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

‘’ Mganga Mkuu wa Wilaya ‘’ maana yake ni daktari ambaye ni msimamizi mkuu wa huduma za afya katika Halmashauri.

“Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri” maana yake ni timu ya kitaalamu ya uendeshaji wa shughuli za afya kwenye Halmashauri iliyoanzishwa chini kifungu cha 13 cha Hati Rasmi hii.

“Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa” maana yake ni timu ya wataalamu wa afya, inayosimamia shughuli zote za huduma za afya mkoani;

“Timu ya uendeshaji wa Huduma za Afya ya Hospitali “maana yake ni timu ambayo inawahusisha viongozi wataalam au wakuu wa sehemu au vitengo kwenye hospitali ya Wilaya;

‘’ Vituo vya Kutolea Huduma ‘’ maana yake ni pamoja na Hospitali, kituo cha afya, kliniki ya tiba, zahanati, maabara ya afya, kituo cha uzazi na uuguzi na pia vituo vingine vilivyoanzishwa kwa ajili ya kutoa huduma za afya.

“Wadhifa wa kisiasa” maana yake ni kuwa na madaraka ya kuteuliwa au kuchaguliwa kwenye chama chochote cha kisiasa kilichoandikishwa chini ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992.

‘’ Zahanati ‘’ maana yake ni kituo cha kwanza kinachotoa huduma kinachotambulika na Halmashauri ambacho kipo ndani ya kata ambacho hutoa huduma kwa wagonjwa wa nje ikiwa ni pamoja na huduma za mama na mtoto na kinaweza kuwa na vitanda vinne kwa ajili ya uangalizi wa karibu wa wagonjwa kwa muda usiozidi saa ishirini na nne.

Bodi

4\. (1) Kutakuwa na Bodi itakayojulikana kama Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri ya Wilaya,

(2) Ofisi za Bodi zitakuwa katika eneo la Halmashauri,

Wajumbe wa Mfuko wa Bodi.

5\. (1) Bodi itaundwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Wawakilishi wanne wa watumiaji wa huduma za afya ambao wawili kati yao ni lazima wawe ni wanawake;

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(b) Mwakilishi mmoja kutoka kwa watoa huduma za afya binafsi kwa faida na mmoja kwa watoa huduma binafsi bila faida, walio katika makubaliano ya kutoa huduma na Bodi; na

(c) Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Huduma za Jamii

(d) Afisa Mipango wa Halmashauri wa Halmashauri ya Wilaya;

(e) Mganga Mkuu wa Wilaya, ambaye atakuwa Katibu wa Bodi ;

(f) Mwakilishi mmoja toka hospitali ya Wilaya au hospitali teule; na ;

(g) Mwakilishi kutoka Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya Mkoa.

(2) Mwenyekiti atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe wa kifungu kidogo (1) (a), (b) na (c) hapo juu.

(3) Wajumbe waliotajwa katika aya (a) (b) na (c) mbali na wajumbe na wajumbe waliotajwa katika aya (d),(e),(f) na (g) za kifungu kidogo cha (1) watakuwa na haki ya kupiga kura katika maamuzi ya Bodi.

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(4) Wajumbe wengine wanaweza kualikwa kama kutakuwa na ulazima wa kufanya hivyo; lakini hawatakuwa na uwezo wa kupiga kura au kufanya maamuzi.

Sifa za kuwa mjumbe wa Bodi.

6 (1) Mtu anaweza kugombea nafasi ya ujumbe wa Bodi kama atakuwa na sifa zifuatazo :

(a) ni lazima awe raia wa Tanzania, Sharti hili si lazima kwa wajumbe kutoka Mashirika yasiyo ya Kiserikali;

(b) awe na umri kuanzia miaka ishirini na moja (21) na kuendelea,

(c) awe amehitimu elimu ya sekondari; yaani kidato cha nne na kuendelea; na

(d) asiwe na wadhifa wowote wa kisiasa toka chama chochote cha siasa.

(e) awe mwanachama hai wa mfuko wa jamii

(f) Asiwe ametiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai

(g) Awe mkazi wa Halmashauri
.

(2) Diwani na mfanyakazi wa Halmashauri, mbali ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Huduma za jamii, hatoruhusiwa kuwa mjumbe wa Bodi, kwa kuwa Bodi ni chombo cha Halmashauri katika masuala ya uwajibikaji na tathmini.

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

Utaratibu wa kupata wajumbe

7.(1) (a) Uhamasishaji ushirikishe viongozi wa Halmashauri na wananchi kwa ujumla katika ngazi ya Wilaya, Kata na Vijiji

(b) Halmashauri kutoa matangazo ya nafasi wajumbe wa Bodi kupitia Wilaya, Kata na Vijiji.

(c) Uchaguzi wa awali: Maombi ya nafasi yatawasilishwa kwenye vijiji na uchaguzi utafanyika mkutano wa hadhara na kusimamiwa na Afisa Mtendaji wa Kata husika.

(d) Uchambuzi wa maombi: Orodha ya waombaji waliochaguliwa yatapelekwa kwenye kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata kwa uchambuzi wa awali kwa kuzingatia sifa na mapendekezo yatapelekwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya.

(e) Uchambuzi wa majina ya wajumbe kutoka ngazi ya Kata yatafanywa na Timu ya Uendeshaji ya Afya ya Halmashauri ya Wilaya kwa kuzingatia sifa na mchakato wa uteuzi wao na kuwasilisha kwenye Timu ya Uendeshaji ya Halmashauri, timu hiyo itahakiki na kuwasilisha mapendekezo hayo kwenye Kamati ya Uchumi na Huduma za Jamii na hatimaye Baraza la Madiwani kuidhinisha.

(f) Uzinduzi rasmi utafanywa na Mkuu wa Wilaya baada ya kupata Hati Rasmi iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Kipindi cha kushika madaraka

8. (1) Wajumbe wa Bodi watakuwa katika madaraka kwa kipindi cha miaka mitatu, kutoka tarehe ya ufunguzi na wataondoka baada ya muda huo lakini wanaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi cha miaka mitatu;

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(2) Mwisho wa kipindi cha muda wa Bodi, Mkurugenzi atatangaza nafasi zilizo wazi na watu wenye sifa hizo watajaza fomu maalum za maombi na kuzirudisha kwenye Halmashauri katika kipindi kitakachotolewa.

(3) Mjumbe wa Bodi anaweza kujiuzulu baada ya kutoa taarifa ya maandishi ya mwezi mmoja kwa Katibu wa Bodi.

(4) (a) Pale ambapo nafasi katika Bodi itakuwa wazi kutokana na kifo, kujiuzulu, ugonjwa, au ulemavu utakaomzuia mtu huyo kushiriki kikamilifu au kwa sababu nyingine yoyote ile, mjumbe mwingine atachaguliwa kuziba nafasi hiyo kwa kipindi kilichobaki.

(b) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha 4 (a), haitaruhusiwa kuchagua mjumbe mwingine iwapo kipindi kilichobaki ni chini ya miezi sita (6)

(5) Mjumbe atakayechaguliwa kutokana na kifungu kidogo cha (4) hapo juu, anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

(6) Uchaguzi wa mwisho wa wajumbe waliochaguliwa kutoka kila mtaa utafanywa na Kikao Kikuu cha Halmashauri kupitia Kamati ya Uchumi na huduma za jamii baada ya kupendekezwa na Timu ya Uendeshaji ya Halmashauri

(7) Bodi itazinduliwa rasmi na Mkuu wa Wilaya baada ya kuidhinishwa na Kikao cha baraza la Madiwani.

(8) Endapo Bodi itashindwa kutekeleza kazi zake, Halmashauri itaionya au kuivunja na kuandaa uchaguzi mpya ndani ya miezi mitatu tangu kuvunjwa.
.

(9) Endapo Bodi itavunjwa, wajumbe wote watapoteza nafasi zao.

(10) Katika kipindi ambacho Bodi imevunjwa, Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri itasimamia shughuli zote za Bodi hadi hapo Bodi mpya itakapoteuliwa.

Vikao vya Bodi

9. (1) Bodi itafanya vikao vyake vya kawaida kila baada ya miezi mitatu kwa mwaka, na vikao vyote vya Bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti au Makamu wake;

(2) Katibu ataitisha kikao maalumu kitakachokuwa cha kawaida cha Bodi kwa maombi yaliyoandikwa na kusainiwa na wajumbe wa bodi wasiopungua theluthi moja na pale inapohitajika.

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(3) Mjumbe yeyote ambaye, bila taarifa au sababu ya msingi, atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi basi atakuwa amepoteza sifa za kuendelea kuwa mjumbe na Halmashauri itatangaza nafasi wazi kwenye nafasi hiyo.

*Akidi ya kikao*

10. (1) Nusu ya wajumbe wote wa kuchaguliwa ndiyo itakuwa akidi ya vikao vyote vya Bodi akiwemo Mwenyekiti au Katibu;

(2) Maamuzi ya idadi ya wajumbe wengi na waliopiga kura ndiyo yatakayokuwa maamuzi ya Bodi.

(3) Upigaji wa kura za siri ndiyo utakuwa utaratibu wa kufikia maamuzi katika vikao vya Bodi.

(4) Kila mjumbe wa Bodi atakuwa na kura moja na pale ambapo itatokea kura kufungana, basi Mwenyekiti wa Bodi atakuwa na kura ya ziada mbali ya kura yake ya kawaida.

Majukumu na Kazi za Bodi

11. (1) Majukumu na kazi za Bodi zitakuwa kama ifuatavyo:-

(a) itahakikisha kuwa jamii inapata huduma bora za afya ambazo inazimudu na zitakazoimarisha afya zao;

(b) itahakikisha kuwa kuna upatikanaji wa rasilimali na mgawanyo wake, kwa kuzingatia mahitaji ya ngazi zote za huduma ya afya na matumizi bora;

(c) itajadili na kurekebisha mipango ya afya na bajeti na kuwasilisha kwa Halmashauri kwa ajili ya kuidhinishwa;

(d) itapokea, itachambua na kuidhinisha taarifa za utekelezaji kutoka kwa Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri;

(e) itabuni vyanzo mbalimbali vya mapato na kukusanya rasilimali za kutosha kuendesha huduma za afya katika Halmashauri;

(f) itashirikiana na Kamati za Afya ndani ya Halmashauri,

(g) itaratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya afya katika Halmashauri; na

(h) itahakikisha kuwa kunakuwepo wafanyakazi wa kutosha kulingana na ikama ya Halmashauri;

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(2) Bodi katika kutekeleza majukumu yake, itapokea na kutekeleza maelekezo ya Halmashauri kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

Uhusiano wa Bodi na wadau na mamlaka nyingine

12. Uhusiano wa Bodi na jamii, wadau na mamlaka nyingine utakuwa kama ifuatavyo;

(a) Bodi itahakikisha kuwa jamii inashirikishwa kikamilifu katika kutambua matatizo, kuweka kipaumbele, kupanga, kuchangia, kufuatilia na kutathmini utoaji wa huduma za afya;

(b) Bodi itawajibika mbele ya Halmashauri ambapo:-

(i) Mipango ya afya ya robo mwaka na mwaka pamoja na taarifa za kitaalam na fedha zinapitiwa na Kamati ya Uchumi, Huduma za Jamii na Kamati ya Fedha na Utawala, na baadaye kuthibitishwa na Baraza la Madiwani;

(ii) Bodi itaendesha shughuli zake kwa utaratibu wa uwazi na ambao utakuza ufanisi kwa Halmashauri na vyombo vyake vingine vya utendaji bila ya Halmashauri kuingilia uhuru wa Bodi;

(c) Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri itakuwa ni chombo cha kitaalamu katika utekelezaji wa maamuzi ya Bodi;

(d) Kuhusiana na Kamati ya Uchumi na Huduma za jamii:

(i) mipango yote na taarifa za maendeleo zitapitia katika Kamati hii, kwa hiyo kamati itakuza uhusiano;

(ii) uhusiano na sekta nyingine utakuzwa na Bodi hasa katika utekelezaji wa maamuzi ya pamoja katika mambo muhimu kwenye Halmashauri;

(e) Uhusiano na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, watoa huduma binafsi na wahisani:

(i) kuwepo kwa wajumbe toka kwenye vyama vya hiari, mashirika yasiyo ya Kiserikali na watoa huduma binafsi ndani ya Bodi kutaleta uhusiano mzuri baina yao;

(ii) Bodi itashiriki katika utafutaji wa mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ikiwemo Halmashauri, vyama vya hiari, jamii na wahisani;

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(f) Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa itatoa msaada wa kitaalamu na ushauri; na

(g) Jukumu la wizara zenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Vijiji na Afya litakuwa ni kuandaa sera ufuatiliaji na kuratibu shughuli za Bodi.

Vyanzo vya mapato vya bodi

13. (1) Vyanzo vya mapato ya Bodi vitakuwa kama ifuatavyo:

(a) Michango ya watu binafsi;

(b) Mfuko wa Afya ya Jamii

(c) Ada za watumiaji huduma; - papo kwa papo

(d) Makusanyo toka Halmashauri;

(e) Wahisani na washirika,

(f) Ruzuku toka Serikali Kuu; na

(g) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

(h) Vyanzo vingine halali vya mapato

(2) Bodi itakuwa na akaunti maalum ya Mfuko wa Afya ya Jamii (Tiba kwa Kadi) ambayo itatunza fedha zitokanazo na michango.

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(3) Wawekaji saini wa akaunti maalumu ya Mfuko wa Afya ya Jamii (Tiba kwa Kadi) pamoja na taratibu nyingine za Mfuko huo zitakuwa kama itakavyoelezwa Katika Sheria Ndogo za uanzishaji Mfuko wa Afya ya Jamii, (Tiba kwa Kadi).

(4) Halmashauri itaajiri au kuteua wahasibu wawili watakao simamia akaunti za afya.

(5) Mganga Mkuu wa Wilaya, atakuwa ndiye mwanzishaji wa malipo yote.

(6) Akaunti hii itakaguliwa kufuatana na taratibu za Fedha za Serikali za Vijiji

.

Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri

14. Kutakuwa na Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri.

Wajumbe

15. Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri itakuwa na wajumbe wafuatao;

(a) Mganga Mkuu wa Wilaya,

(b) Katibu wa Afya wa Wilaya,

(c) Muuguzi Mkuu wa Wilaya,

(d) Afisa Afya wa Wilaya,

(e) Mfamasia wa Wilaya,

(f) Fundi Sanifu wa Maabara wa Wilaya,

(g) Daktari wa Meno wa Wilaya,

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(h) Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya.

Majukumu na kazi za Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya

16 (1) Majukumu na kazi za Timu ya Uendeshaji wa Huduma za afya ya Halmashauri zitakuwa kama ifuatavyo:-

(a) (a) kuandaa mipango kabambe ya afya ambayo itatilia mkazo mahitaji yote ya afya ya Halmashauri kwa kuzingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Mpango wa Afya wa Halmashauri;

(b) kuhakikisha kuwa hospitali, vituo vya afya na jamii vinatekeleza shughuli za afya kama inavyoelekezwa katika mpango kabambe wa Afya wa Halmashauri;

(c) kuhakikisha upatikanaji wa usafiri, dawa muhimu, chanjo, dawa, vifaa tiba, kemikali za maabara katika hospitali, vituo vya afya na zahanati

(d) kuwa tayari kukabiliana na magonjwa ya milipuko, maafa na kupanga mipango ya kudhibiti na kuzuia mambo hayo;

(e) kuhakikisha kuwa watumishi wa afya walio katika ngazi mbalimbali kwenye Halmashauri wanapata nyenzo za kuwawezesha kufuatilia utekelezaji wa shughuli za afya;

(f) kuhakikisha kuwa huduma za afya zinatolewa kulingana na viwango vya Kitaifa;

(g) kuhakikisha kuwa watumishi wa afya wanakusanya takwimu, wanazichambua na kuzitumia katika mipango yao na kutoa mrejesho;

(h) kutambua maeneo ya kuweka kipaumbele, kusimamia na kufanya utafiti wa utendaji kazi katika Halmashauri ;

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(i) kujumuisha na kuchambua taarifa za utekelezaji wa kitaalamu na fedha za robo mwaka na mwaka, halafu kuziwasilisha kwenye Bodi na sekretarieti ya Mkoa kupitia kwa Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa;

(j) kusimamia mikutano ya wataalamu wa afya wanaotoa huduma za afya kwenye Halmashauri ili kuweza kutambua na kuratibu shughuli zote za afya;

(k) kusimamia na kusaidia utoaji wa huduma za afya ambazo ziko mbali kutoka kwenye vituo vya kutolea huduma; na

(l) kufuatilia na kutathimini utekelezaji wa shughuli za afya kwenye Halmashauri

(2) Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri itawajibika kwa Halmashauri.

Uhusiano wa Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri na Kamati au mamlaka nyingine

17 Timu za Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Halmashauri, kwa madhumuni ya kuleta uongozi bora, itashirikiana na Kamati nyingine za afya na mamlaka nyingine ili kuleta mtandao wa utoaji wa huduma bora za afya katika Halmashauri.

Kamati ya Usimamizi ya Hospitali

18. Kutakuwa na Kamati ya Usimamizi ya Hospitali katika kila hospitali iliyo chini ya Halmashauri.

Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi ya Hospitali

19 (1) Wajumbe wa kamati ya Usimamizi ya Hospitali watakuwa kama ifuatavyo:-

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(a) wawakilishi watatu kutoka watumiaji wa huduma za hospitali,

(b) wajumbe wawili kutoka kwenye kamati za vituo vya afya na zahanati

(c) mjumbe mmoja kutoka kwa watoa huduma za afya binafsi bila faida; na

(d) Mjumbe mmoja kutoka kwa watoa huduma za afya binafsi kwa faida.

(2) Kutakuwa na Sekretarieti ambayo itaundwa na wajumbe wafuatao;-

(a) mwakilishi toka Halmashauri aliyeteuliwa na Mkurugenzi wa Wilaya

(b) mganga Mkuu Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya, ambaye atakuwa Katibu; na

(c) Muuguzi mkuu wa Hospitali ya Wilaya

(d) mwakilishi mmoja toka katika ofisi ya Mganga Mkuu

(3) Theluthi moja ya wajumbe wa Kamati ya Usimamizi lazima wawe ni wanawake.

(4) Wajumbe waliotajwa katika kifungu kidogo (1) hapo juu ndiyo watakaokuwa na haki ya kupiga kura.

(5) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati watachaguliwa kutokana na wajumbe wa kifungu kidogo cha (1) hapo juu;

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(6) Mjumbe wa Kamati ya Usimamizi wa Hospitali anaweza kujiuzulu baada ya kutoa taarifa ya maandishi ya mwezi mmoja kwa Katibu.

(7) Kamati ya Usimamizi wa Hospitali inaweza kumkaribisha mtu yeyote kuhudhuria vikao vyake kama kutakuwa na ulazima wa kufanya hivyo, lakini mtu huyo hatoruhusiwa kushiriki katika kupiga kura au kupitisha maamuzi ya Kamati.

Sifa za wajumbe wa Kamati ya usimamizi ya Hospitali

20 Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi ya Hospitali wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

(a) Awe raia wa Tanzania, sharti hili halitawahusu wajumbe kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali;

(b) Awe na umri usiopungua miaka ishirini na moja na kuendelea

(c) Awe amehitimu elimu ya sekondari au zaidi

(d) Awe na akili timamu;

(e) Awe mkazi wa Halmashauri ya Wilaya.

(f) Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai

(g) .Asiwe na wadhifa wowote wa kisiasa kupitia chama chochote cha siasa.

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

Taratibu za uchaguzi

21 (1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2) na (3) cha kifungu hiki, wajumbe wote wa Kamati ya Usimamizi ya Hospitali watachaguliwa kwa kuzingatia sifa zao na kwa uwazi.

(2) Nafasi za uongozi katika Kamati ya Usimamizi ya Hospitali zitatangazwa katika gazeti linalopatikana katika Halmashauri pamoja na kutangazwa katika mbao za matangazo na mikusanyiko ya watu na watu wenye sifa zinazohitajika na nia ya kufanya hivyo watapeleka maombi kwa Mkurugenzi wa Halmashauri;

(3) Uchaguzi wa wajumbe utafanyika kwenye mtaa na kusimamiwa na Afisa Mtendaji wa Mtaa au Afisa Mtendaji wa Kata au afisa yeyote atakayeteuliwa na Halmashauri;

(4) Uchaguzi utafanyika kwa njia ya mkutano wa hadhara;

(5) Baada ya uchaguzi, orodha ya wajumbe waliochaguliwa itachanganuliwa na Timu ya Uendeshaji ya Huduma za Afya ya Halmashauri na itapelekwa kwa Timu ya Uendeshaji ya Halmashauri;

(6) Uteuzi wa mwisho utafanywa na Baraza la Madiwani kupitia Kamati ya Uchumi na Huduma za Jamii baada ya kupendekezwa na Timu ya Uendeshaji ya Halmashauri.

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(7) Wajumbe wenye sifa zinazohitajika ndiyo watachaguliwa kuwa wajumbe wa Kamati ya Usimamizi ya Hospitali.

Uzinduzi rasmi

22 Kamati ya usimamizi ya Hospitali itazinduliwa rasmi sanjari na uzinduzi wa Bodi ya Halmashauri

Vikao vya Kamati ya Usimamizi ya Hospitali

23. (1) Kamati ya Usimamizi ya Hospitali itafanya vikao vyake vya kawaida kila baada ya miezi mitatu katika sehemu; tarehe na muda utakaopangwa na Mwenyekiti kwa kushirikiana na Katibu.

(2) Mwenyekiti wa Kamati kwa kushirikiana na Katibu wake anaweza kuandaa kikao cha dharura kama itakavyohitajika.

(3) Taarifa ya Kikao itapelekwa kwa kila mjumbe wa Kamati ya Usimamizi ya Hospitali wiki moja kabla ya kikao kuanza, baada ya kuwafahamisha kwa maandishi madhumuni, tarehe na muda wa kikao.

Majukumu na kazi za Kamati ya Usimamizi ya Hospitali

24 1 Majukumu na kazi za Kamati zitakuwa kama ifuatavyo:

(a) itasimamia rasilimali za hospitali ,

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(b) itapokea, itajadili na kupitisha mapendekezo ya mipango ya hospitali na bajeti na kuipeleka Halmashauri kwa ajili ya kuthibitishwa kupitia Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri,

(c) itapokea na kujadili taarifa za utekelezaji zilizoandaliwa na Timu ya Usimamizi ya Hospitali,

(d) itabuni vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kuendesha huduma za afya,

(e) itashirikiana na Kamati nyingine za afya na mashirika mbalimbali katika utoaji na uboreshaji wa huduma za afya,

(f) itapendekeza kuhusu upatikanaji wa watumishi na mafunzo yao ili kuleta ufanisi katika hospitali, na

(g) kutoa mrejesho kwa jamii kuhusu uendeshaji wa hospitali na mipango ya maendeleo.

Utoaji taarifa na uwajibikaji

25. Kamati ya Usimamizi ya Hospitali itatoa taarifa na kuwajibika mbele ya Halmashauri kupitia Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri.

Uhusiano wa Kamati ya Usimamizi ya Hospitali na Kamati au mamlaka nyingine

26. Kamati ya Usimamizi ya Hospitali, kwa madhumuni ya kuleta uongozi bora, itashirikiana na Kamati nyingine za afya ili kuleta mtandao wa utoaji wa huduma bora za afya katika Halmashauri.

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

Vyanzo na usimamizi wa mapato

27. (1) Vyanzo vya mapato vya Kamati ya Usimamizi ya Hospitali vitakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Fedha itakayotengwa kwa ajili ya Hospitali katika bajeti ya Halmashauri zilizopatikana kupitia Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri,

(b) Mapato yatokanayo na uchangiaji wa Huduma za Afya yaliyotengwa na Bodi kwa ajili ya hospitali,

(c) Ruzuku na michango itakayotolewa na Halmashauri, na Serikali Kuu; na

(d) Vyanzo vingine halali vya Mapato.

(2) Kutakuwa na akaunti ya Hospitali ambayo itakaguliwa kwa kuzingatia Kanuni za Fedha za Serikali za Vijiji.

(3) Watia saini watakuwa katika makundi mawili kundi “A” Wataalamu na kundi “B” Jamii

(4) Mganga Mkuu wa Wilaya, atamteua mmoja wa wahasibu wake kusimamia akaunti ya Hospitali chini ya uangalizi wa Mganga Mfawidhi

(5) Mganga Mfawidhi ataanzisha Hati zote za malipo zitakazohusiana na Shughuli za hospitali.

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

Bodi ya Hospitali Kufanya kazi za Kamati

28. Pale ambapo hakuna hospitali ya wilaya ya Serikali shughuli za kamati ya Usimamizi ya Hospitali zifanywe na Bodi ya usimamizi ya Hospitali Teule.

Kamati ya Kituo cha Afya

29. (1) Kutakuwa na Kamati ya Kituo cha Afya, ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mjumbe mmoja kutoka kwa watoa huduma za afya binafsi kwa faida;

(b) Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya, ambaye atakuwa Katibu;

(c) Wawakilishi watatu watumiaji wa huduma za Kituo watakaochaguliwa mmoja kutoka kila kata; pale ambapo kuna kata zaidi ya tatu, basi wataingia kwa kupokezana.

(d) Mjumbe mmoja kutoka kwa watoa huduma za afya binafsi bila faida;na

(e) Mtaalam mmoja kutoka kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu (c), mwakilishi wa kupokezana atakaa kwenye Kamati kwa kipindi cha mwaka mmoja.

(3) Kamati ya Kituo cha Afya inaweza kumualika mtu yeyote ambaye si mjumbe wa Kamati kuhudhuria katika vikao vyake, lakini mtu huyo hatashiriki katika kupiga kura au kutoa maamuzi ya Kamati;

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(4) Mwenyekiti na Makamu wa Mwenyekiti watachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe wanaopiga kura ;

(5) Theluthi moja ya wajumbe wote ni lazima wawe wanawake.

Sifa za Wajumbe

30. Mjumbe wa Kamati ya Kituo cha Afya atapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

(a) Awe raia wa Tanzania, sharti hili haliwahusu wajumbe kutoka mashirika yanayotoa huduma za afya yasiyo ya kiserikali,

(b) awe na umri si chini ya miaka ishirini na moja (21) na kuendelea

(c) awe ni mkazi wa Halmashauri ya Wilaya

(d) awe na akili timamu.

(e) awe amehitimu elimu ya msingi au zaidi na anajua kusoma na kuandika kwa kiswahili;
.

(f) asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai

(g) asiwe na wadhifa wa kisiasa toka katika chama chochote cha siasa.

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

Taratibu za Uchaguzi

31. (1) Matangazo: Afisa Mtendaji wa Kata atatoa matangazo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya wawakilishi wa watumiaji huduma za vituo vya Afya na Zahanati

(a) Maombi yatafanyika kwenye Vijiji akisimamia Mtendaji wa Mtaa na uchaguzi utafanyika kwenye mkutano wa hadhara na atachaguliwa mjumbe mmoja tu

(b) Uchambuzi wa waombaji kutoka katika kila Kata yatachambuliwa na Timu ya Uendeshaji ya kila Kata ambapo Kituo cha Afya na Zahanati ipo.

(c) Kamati ya Maendeleo ya Kata itafanya uchaguzi na kuwasilisha orodha ya wagombea wote kwenye Bodi ya Afya ya Halmashauri na Bodi itawasilisha kwenye Baraza la Madiwani kwa kuidhinishwa

Muda wa kukaa madarakani

32. (1) Mjumbe wa kamati ya Maendeleo ya Kata mbali ya mwakilishi wa kupokezana, atakaa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu, na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu isiyozidi vipindi viwili.

(2) Mjumbe wa Kamati anaweza kujiuzulu baada ya kutoa taarifa ya maandishi ya mwezi mmoja kwa Katibu.

(3) Endapo mjumbe atajiuzulu nafasi yake itajazwa; na mjumbe atakayejaza nafasi hiyo atakaa kwenye uongozi kwa kipindi kilichobaki, lakini anaweza kuchaguliwa tena kuendelea kwa kipindi kingine.

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(4) Mjumbe atakayejaza nafasi katika kifungu kidogo cha (3) hatoruhusiwa kufanya hivyo kama kipindi kilichobaki kitakuwa chini ya miezi sita.

(5) Iwapo Kamati ya Kituo cha Afya itashindwa kutekeleza majukumu yake basi Halmashauri inaweza kutoa onyo au kuivunja na kuandaa uchaguzi mpya ndani ya miezi mitatu.

Vikao vya kamati

33 (1) Kamati ya Kituo cha Afya itafanya vikao vyake vya kawaida kila baada ya miezi mitatu katika sehemu, siku na muda utakaopangwa.

(2) Mwenyekiti wa Kamati kwa kushirikiana na Katibu anaweza kuandaa kikao cha dharura pale tu atakapoomba au kuombwa kufanya hivyo kimaandishi na kupata idhini ya wajumbe wasiopungua theluthi moja ya wajumbe wote.

(3) Katibu atatoa taarifa ya maandishi ya kikao kwa kila mjumbe wa Kamati wiki moja kabla ya kikao, kwa kumfahamisha madhumuni, siku na muda wa kikao.

Kazi za Kamati

34. (1) Kazi za Kamati ya Kituo cha Afya zitakuwa kama zifuatavyo:-

(a) Itapokea na kujadili taarifa za utekelezaji zilizotayarishwa na Timu ya Uendeshaji wa Kituo cha Afya;

(b) Itabuni vyanzo mbalimbali vya mapato na kukusanya rasilimali za kutosha kuendeshea huduma za Kituo cha Afya;

(c) Kamati itashirikiana na washirika wengine katika utoaji

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

na uboreshaji wa huduma za afya;

(d) Itaimarisha miundombinu endelevu na usambazaji wa uhakika wa dawa na huduma za afya;

(e) Itashauri na kutoa mapendekezo kwa Bodi kuhusu watumishi katika nyanja za ajira, mgawanyo, mafunzo, maendeleo na motisha;

(f) Itasaidia Timu ya Uendeshaji ya kituo cha Afya katika kupanga na kusimamia mambo ya afya ya Jamii katika eneo lake kama sehemu ya mpango wa Maendeleo ya kata; na

(g) Itasimamia upatikanaji wa dawa muhimu, kemikali za maabara na vifaa tiba.

(2) Kamati ya Kituo cha Afya itawajibika kutokana na shughuli zake za kila siku kwa Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri

Uhusiano na taasisi nyingine

35. (1) Katika kutekeleza kazi zake, Kamati ya Kituo cha Afya:

(a) itahakikisha kuwa mahitaji ya afya ya jamii yanafanyiwa kazi;

(b) itatafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ;

(c) itakuwa na daftari la usajili wa wachangiaji wa Mfuko wa Afya wa Jamii;

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(d) itajenga na kuimarisha ushirikiano na uwiano na taasisi nyingine kwenye Halmashauri;

(e) itahakikisha kuwa Kamati ya Zahanati inawakilishwa kwenye Kamati ya Kituo cha Afya; na

(f) itahakikisha kuwa Kamati ya Kituo cha Afya inawakilishwa kwenye Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri;

(2) Timu ya Uendeshaji Huduma za Afya ya Halmashauri itatoa ushauri wa kitaalamu kwa Kamati ya Kituo cha Afya.

Kamati ya Afya ya Kata

36. Kutakuwa na Kamati ya Afya ya Kata.

Sura ya 409,

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

Wajumbe wa Kamati Sura 409 .

37. (1) Kamati ya Afya ya Kata itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Diwani anayewakilisha kata husika;

(b) Afisa Mtendaji wa Kata;

(c) Mwalimu Mkuu mmoja kutoka kwenye shule ya msingi iliyopo kwenye Makao Makuu ya kata husika;

(d) Wajumbe wawili wanaoiwakilisha jamii husika ambapo mmoja wao ni lazima awe mwanamke;

(e) Tabibu wa Afya Mfawidhi au Tabibu Mfawidhi Msaidizi; wa kituo cha Afya, ambaye atakuwa Katibu wa Kamati;

(f) mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kutokana na watu waliopendekezwa na serikali za mtaa zilizomo ndani ya eneo la kata; na

(g) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kutoka kwenye vyama vya kijamii vilivyomo kwenye kata.

(2) Mwenyekiti wa Kamati ya Afya ya Kata atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe hapo juu.

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(3) Endapo Kamati ya Afya ya Kata itashindwa kutekeleza kazi zake, Halmashauri itatoa onyo au kuivunja na kufanya utaratibu wa uchaguzi wa wajumbe wengine katika muda usiozidi miezi mitatu.

Sifa za Wajumbe wa Kamati ya Afya ya Kata

38 Sifa za Wajumbe wa Kamati ya Afya Kata zitakuwa ni kama zifuatavyo:-

(a) awe raia wa Tanzania, sharti hili haliwahusu wajumbe kutoka mashirika yanayotoa huduma za afya yasiyo ya kiserikali.

(b) awe na umri wa miaka ishirini na moja na kuendelea.

(c) awe na akili timamu

(d) awe na elimu ya msingi au zaidi na ajue kusoma na kuandika .

(e) asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai.

(f) asiwe na wadhifa wa kisiasa toka chama chochote cha siasa

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

Kazi na majukumu ya Kamati

39. (1) Kamati ya Afya ya Kata itakuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) kuwahamasisha na kuandaa jamii kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii;

(b) kuandaa orodha na kuratibu idadi ya wajumbe wa Mfuko wa Afya ya Jamii;

(c) kusimamia ukusanyaji wa michango ya Mfuko;

(d) kuratibu viwango vya uchangiaji kwenye huduma za afya;

(e) kupitia utendaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii na kutoa mapendekezo na ufumbuzi;

(f) kuanzisha na kuratibu mipango ya Afya ya Jamii; na

(g) kuendesha mikutano ya wajumbe wa Mfuko wa Afya ya Jamii.;

(2) Kamati ya Afya ya Kata, itakaa kila baada ya miezi mitatu, na katibu atatoa taarifa ya maandishi wiki moja kabla ya siku ya Kikao.

(3) Wajumbe wa Kamati ya Afya ya Kata watakaa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu lakini anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi cha miaka mitatu na isiyozidi vipindi viwili.

Kamati ya zahanati

40 Kutakuwa na kamati ya Zahanati.

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

Wajumbe wa Kamati ya Zahanati

41 (1) Kamati ya Zahanati itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) wajumbe wa kuchaguliwa ambao watapiga kura:-

(i) wajumbe watatu kutoka miongoni mwa jamii inayohudumiwa na zahanati husika;

(ii) mjumbe mmoja atakayewakilisha taasisi inayotoa huduma za afya bila faida;

(iii) mjumbe mmoja atakayewakilisha taasisi inayotoa huduma ya afya kwa faida;

(b) Kutakuwa na Sekretarieti ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(i) Mtaalam mmoja kutoka kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata;

(ii) Mwakilishi mmoja kutoka kwenye Kamati ya Serikali ya Mtaa;

(iii) Mganga mfawidhi wa zahanati ambaye atakuwa Katibu, pale ambako kutakuwa na Zahanati zaidi ya moja, kutakuwa na utaratibu wa kupeana zamu;

(2) Idadi ya wajumbe wanawake si chini ya theluthi moja ya wajumbe wote.

(3) Mwenyekiti wa Kamati ya Zahanati atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe walioelezwa kwenye kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(4) Wajumbe wa Sekretariati hawatakuwa na haki ya kupiga kura.

Taratibu za kuwapata wajumbe na muda wa kukaa madarakani

42 (1) Wajumbe wa Kamati ya Zahanati watachaguliwa kwa kufuata utaratibu ufuatao:-

(a) Afisa Mtendaji wa Kata atatangaza nafasi wazi;

(b) mapendekezo ya majina ya wagombea yatawasilishwa kwenye Timu ya Wataalamu ya Kata ambapo yatachanganuliwa kabla ya kuwasilishwa kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata; na

(c) Kamati ya Maendeleo ya Kata itapendekeza majina ya wajumbe na kuyawasilisha kwenye Halmashauri kupitia kwenye Bodi ili kuidhinishwa.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Zahanati watashika madaraka kwa kipindi cha miaka mitatu, isipokuwa kwa wajumbe ambao watashika nafasi zao kwa kupokezana, ambao watakaa kwa mwaka mmoja. Wajumbe wengine wanaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu na isiyozidi vipindi viwili.

Vikao vya Kamati ya Zahanati

43 (1) Kamati ya Zahanati itafanya vikao vyake vya kawaida kila baada ya miezi mitatu isipokuwa kunaweza kukafanyika kikao cha dharura kama itahitajika.

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(2) Akidi ya mkutano itakuwa ni nusu ya wajumbe wote wa kuchaguliwa ikiwa ni pamoja na Mwenyekiti na Katibu.

(3) Taarifa ya Kikao itatolewa kwa maandishi na Katibu, wiki moja kabla ya siku ya kikao.

Sifa za Wajumbe

44 Mjumbe wa Kamati ya Zahanati anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

(a) awe raia wa Tanzania, sharti la uraia halitawahusu wajumbe wanaotoka katika mashirika yasiyo ya kiserikali.

(b) awe na umri wa miaka ishirini na moja na kuendelea

(c) awe na elimu ya msingi au zaidi na anajua kusoma na kuandika

(d) anawakilisha watumiaji wa zahanati ;

(e) awe na akili timamu

(f) asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai.

(g) asiwe na wadhifa wa kisiasa kutoka chama chochote cha siasa.

Kazi na majukumu ya Kamati ya Zahanati

45. (1). Kamati ya Zahanati itakuwa na kazi na majukumu yafuatayo:-

(a) itahakikisha kuwa jamii kwenye eneo lake inapata huduma bora na rahisi za afya;

(b) itapokea, itajadili na kupitisha mipango na bajeti ya zahanati;

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(c) itatafuta na kubainisha vyanzo vya mapato ya kuendeshea huduma za Afya kwenye zahanati;

(d) itashirikiana na kamati nyingine za afya na mashirika katika utoaji na uboreshaji wa huduma za afya;

(e) itaendeleza miundombinu endelevu ya afya na mgao wa uhakika wa mahitaji muhimu;

(f) itashauri na kupendekeza kuhusu masuala ya watumishi yanayohusu ajira, mafunzo, mgawanyo na motisha;

(g) itasaidia na kuiwezesha Timu ya Uendeshaji ya Zahanati kupanga na kusimamia shughuli mbalimbali za jamii katika eneo lake kwa kuzingatia Mipango ya Maendeleo ya Kata;

(h) itawasilisha mipango yake ya robo mwaka, nusu mwaka na ya mwaka mzima kwenye Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri; na

(i) itafanya mambo mengine muhimu kama itakavyoagizwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata.

(2) Kamati ya Zahanati itawajibika kwa Bodi ya Afya ya Halmashauri.

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

Uhusiano na Sekta nyingine

46. Ili kuboresha utendaji wa kazi, Kamati itakuwa na mahusiano na sekta nyingine kama ifuatavyo:-

(a) itahakikisha kuwa Jamii inawakilishwa na wajumbe kwenye Kamati ya Zahanati ili kuhakikisha kuwa mahitaji ya jamii yanashughulikiwa;

(b) itapewa ushauri wa kitaalamu na Timu ya Uendeshaji wa Huduma ya Afya ya Halmashauri;

(c) itawakilishwa kwenye Kamati ya Kituo cha Afya kwa mtindo wa kupokezana ili kuhakikisha kuwa mambo ya Zahanati yanazingatiwa; na

(d) Itashirikiana na wadau wengine kwa kutafuta mapato, kujenga na kuimarisha ushirikiano.

Mapato ya Zahanati

47. (1) Vyanzo vya mapato ya Kamati ya Zahanati vitakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Michango ya jamii;

(b) Mfuko wa Afya ya Jamii; (Tiba kwa Kadi)

(c) Ruzuku kutoka Halmashauri;

(d) Wahisani na washirika;

(e) Ruzuku kutoka Serikali Kuu,

(f) Mfuko wa Bima ya Afya,

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

(g) Gharama ya dawa/Vifaa tiba kwa asilimia hamsini (50%)

(h) Vyanzo vingine halali vya mapato.

(2) Bila kuathiri kifungu kidogo cha 1(b) ambacho mapato yake yanasimamiwa na Bodi ya Mfuko wa Afya ya Jamii, mapato mengineyo ya Zahanati yatahifadhiwa katika Akaunti ya zahanati na kusimamiwa na Mganga Mfawidhi wa Zahanati.

Bodi kuwa na a uwezo wa kukagua

48. Bodi, kupitia Halmashauri, itakuwa na madaraka ya kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa huduma za afya zinazotolewa kwenye eneo la Halmashauri.

Makosa

49. Itakuwa ni makosa kwa mtu yeyote ambaye;:-

(a) atakwenda kinyume na masharti ya Hati Rasmi hii; au

(b) atafanya kitendo chochote ambacho kitazuia Bodi, Kamati au Timu yoyote kufanya kazi zake kwa ufanisi; au

(c ) atatumia vibaya mali na rasilimali za Bodi au Kamati na kusababisha kutofikia

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*

malengo ya Bodi; au

(d) atashindwa kwa kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Hati Rasmi hii,

Adhabu

50. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlele imebandikwa katika Sheria hizi Ndogo kutokana na Azimio la kikao cha Halmashauri ya Wilaya ya Mlele kilichoketi tarehe 17 mwezi 07 mwaka 2015 na lakiri imebandikwa mbele ya:-

GODWIN L. BENNE,
*Mkurugenzi (W),*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.*

DUES J. BUNDALA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.*

NAKUBALI,

Dodoma,
09 Januari, 2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)
*Waziri wanchi-or-Tamisemi.*

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea)*